

JINA.....NAMBARI.....

DARASA.....SAHIHI.....

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Juni 2017

Muda: Saa 2  $\frac{3}{4}$

SHULE YA UPILI YA SACHO

MTIHANI WA JUNI

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2  $\frac{3}{4}$

Maagizo

- Jibu maswali **manne** pekee.
- Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
- Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizobaki; yaani: Tamthilia, Hadithi Fupi, Ushairi na Fasihi Simulizi.
- Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
- Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa.**
- Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

SEHEMU	SWALI	UPEO
USHAIRI		
RIWAYA		
TAMTHILIA		
HADITHI FUPI		
FASIHI SIMULIZI		

## SEHEMU A: USHAIRI

### LAZIMA (alama 20)

1.Soma shairi hili kisha ujibu maswali yafuatayo. (alama 20)

Nikumbuke mwanangu,  
Kila asubuhi unapoamka,  
Kwenda kazini,  
Unapochukua sabuni ya kunukia,  
Na dodoki jororo

Na kopo la koligeti,  
Kwenda kukoga hamamuni,  
Penye maji ya bomba,  
Yaliyochunjwa na kutakaswa,  
Mororo...

Kumbuka nyakati zile,  
Za staftahi ya sima na mtama,  
Ndizi na nagwa,  
Kwa mchicha na kisamvu,  
Na ulipokwenda choo,  
Ulilia kwa uchungu,

Nikumbuke,  
Unapotoka nyumbani asubuhi maridadi,  
Katika suti ya moto,  
Miwani ya pembe,  
Viatu vya Paris,  
Saa ya dhahabu,  
Unapong'oka kwenda kazini,  
Katika Volvo,  
Katika njia iliyosakafiwa.

Kumbuka,  
Nyakati zile,  
Mimi ni mamako,  
Tulivyojidamka,  
Mara tu kwale wa kwanza,  
Alipoanza kukoroma,  
Jogoo wa kwanza hajawika,  
Mimi nikachukua mundu na panga,  
Mamako jembe na shoka,  
Tukaelekea porini,  
Kufyeka na kuchimbua,

Na hubaki wajiandaa kwenda shule..  
Nikumbuke,  
Saa za jioni,  
Unapovalia kitanashati

Maswali

- a) Thibitisha kuwa utungo huu ni shairi (alama 4)
- b) Fafanua toni ya utungo huu (alama 2)
- c) Huku ukitoa mifano, linganua kati ya mistari toshelezi na mistari mishata (alama 4)
- d) Eleza maudhui yoyote matatu yanayojitokeza (alama 6)
- e) Eleza sifa zozote mbili za nafsi nenewa (alama 4)

## **SEHEMU B: RIWAYA**

### **Kidagaa kimemwozea (alama 20)**

2... Walimpiga kituku kama nyoka. Nikumbukapo naona fundo chungu moyoni...

- (a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
- (b) Taja mbinu mbili za lugha katika dondoo hili (alama 2)
- (c) Kwa kurejelea dondoo hili fafanua maudhui yanayojitokeza (alama 2)
- (d) Fafanua maudhui uliyotaja hapo juu (c) kwa kutoa mifano kwa riwaya nzima (alama 12)

Au

3. Fafanua mbinu hizi kama zinavyojitokeza katika riwaya. (alama 20)

- (a) Barua
- (b) Kinaya
- (c) Sadfa
- (d) Mbinu rejeshi
- (e) Majazi

## SEHEMU C : TAMTHILIA

### TAMTHILIA YA MSTAHIKI MEYA (Timothy Arege)

4. “Najua ni kazi ila usisahau pia kwamba wafanyikazi wamegoma.”
- (i) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (ii) Wahusika wawili wanaohusishwa na dondoo hili wamebaidika kama ardhi na mbingu. Thibitisha. (alama 16)

Au

5. (b) “Unaona sasa? Mlinidanganya.” Kauli hii ni idhibati tosha kuwa, Mstahiki Meya alidanganyika na kuongozwa na falsafa zisizo na mashiko katika uongozi wake. Tetea ukweli huu. (alama 20)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

### Damu Nyeusi na hadithi nyingine (alama 20)

6. “Mara walianza ama kuniashiria kidole au kutuashiria..Macho wameyakodoa kwa tuhuma. Walisemezana kwa Mizengwe.”
- (a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- (b) Eleza kwa tafsihi yaliyotokea baada ya dondoo hili. (alama 4)
- (c) Kwa kurejelea hadithi hii, eleza masuala makuu yanayoibuka katika kisa hiki. (alama 12)

Au

- 7.
- (a) Jadili ufaafu wa anwani “**Shaka ya Mambo**”. (alama 10)
- (b) Fafanua jazaanda ya **Kikaza** kwa mujibu wa hadithi husika. (alama 10)

## **SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

### **FASIHI SIMULIZI (alama 20)**

- 8.(a) Linganisha fasihi simulizi na fasihi andishi.(alama 5)
- (b) Taja asili ya lakabu.(alama 5)
- (c) Fafanua sifa tano za maghani.(alama 5)
- (d) Mtafiti huenda akapatwa na changamoto nyanjani, fafanua.(alama 5)

for free revision papers visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)